USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

U.S. President's Malaria Initiative







# USAID | TANZANIA

## MRADI WA OKOA MAISHA DHIBITI MALARIA (OMDM)

Mradi wa OMDM unalenga kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa maambukizi ya ugonjwa wa malaria katika ngazi zote za Serikali ya Tanzania (GoT), kuongeza ubora wa matokeo ya afua zinanzotumika dhidi ya Malaria kwa kuboresha ulengaji  na utekelezaji wa afua kwenye maeneo husika, kuboresha mbinu za kudhibiti vyanzo vya maambukizi na kukabiliana na milipuko, na kutoa takwimu muhimu kwa serikali na wadau kwa ajili ya maendeleo na maamuzi ya  kisera ya mpango wa kudhibiti malaria.

OMDM inatoa msaada wa kiufundi kwa Mpango wa Kitaifa wa Kudhiiti Malaria (NMCP) na Mpango wa Kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP) katika maeneo makuu manne:

- kudumisha matokeo kupitia ujumuishaji wa mradi, umiliki wa ndani na uimarishaji wa uwezo:
- kuongeza matumizi ya takwimu kwa ajili ya kufanya maamuzi:
- kuendeleza mipango iliyopo:
- kufanya jinsia kuwa muhimu kwa mbinu za kiufundi na kiutendaji; na kutumia maarifa na mitandao ya kitaifa na kimataifa katika utekelezaji.

## Eneo la kwanza: Kuhakikisha Ufuatiliaji wa Malaria Umeboreshwa

Eneo la kwanza la mradi linazingatia kipengele kikuu cha kwanza cha Mfumo wa Matokeo wa OMDM wa ufuatiliaji wa magonjwa. Mradi umejengwa juu ya muktadha wa kiprogramu wa mifumo iliyopo ya ufuatiliaji ya Tanzania, ikijumuisha mfumo wa taarifa za usimamizi wa afya (HMIS) / ya wilaya mfumo wa ukusanyaji wa taarifa (DHIS2), tafiti pamoja na mifumo inayotumika

na mpango wa kudhibiti malaria katika kufuatilia na kutathimini hali ya maambukizi na utendaji wa sekta ya afya, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa malaria.



## Eneo la pili: Kuboresha ufuatiliaji na utafiti wa mbu waenezao malaria

Ufuatiliaji na utafiti wa mbu wanaoeneza malaria ni shughuli kuu inatolenga kuangalia matokeo ya matumizi afua mbalimbali zinazolenga kumwanagamiza au kumdhibiti mbu wa malaria. Ufuatiliaji huu unajumuisha ufutiliaji wa utendaji wa viua-dudu vitumikavyo kwenye vyandarua, kupuliza ukoko ndani ya nyumba na kwenye mazalia ya mbu. Pamoja na kufuatilia ubora wa viuadudu hivi, pia tafiti zinafanywa kuangalia ufanisi wake katika kudhibiti mbu wa malaria na kama hawa mbu wameanza kujenga usugu dhidi hivi viuadudu. OMDM ikisihiririkiana na wadau wengine ndani ya nchi imekuwa ikitoa usaidizi wa kiufundi kwa NMCP na ZAMEP, ili kuweka takwimu ya ufuatiliaji na utafiti wa mbu waenezao malaria ambazo zitasaidia kufanya mamamuzi sahihi katika mipango ya kudhibiti malaria nchini. Vilevile OMDM imekuwa ikishiriki katika kuwezesha mikutano ya wataalam wa kudhibiti mbu wa malaria ya kila robo mwaka ya NMCP na ZAMEP, na kusaidia utayarishaji na usahihishaji wa mara kwa mara wa mipango ya kisera na miongozo mbalimbali itumikayo katika udhibiti wa mbu waenezao malaria

## Eneo la tatu: Kuboresha Ufuatiliaji wa Ufanisi wa Dawa zitumikazo kutibu malaria

Ili kupunguza tishio la upunguaji wa ufanisi wa dawa za kutibu malaria inayoathiri udhibiti wa ugonjwa wa malaria, NMCP na ZAMEP, na wadau lazima kuwa na mpango wa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa dawa hizi. Ufuatiliaji huu unafanywa kupitia tafiti za ufanisi wa kimatibabu (TES)— unaowezesha kupata taarifa kwa wakati, mwafaka, zinazokidhi mahitaji, zilizo sahihi na zinazoeleweka na kuaminika. OMDM inashirikiana na wadau wa ndani ili kufanikisha kutoa msaada wa kitaalam kwa NMCP na ZAMEP ili kuhakikisha takwimu za TES zinapatikana katika mifumo ya NMCP; kuhakikisha TES inafanyika kila mwaka Tanzania Bara na Zanzibar; kuwezesha mikutano ya robo mwaka ya NMCP na ZAMEP TES TWGs; na kusaidia uandaaji na usasishaji wa mara kwa mara wa mipango ya kisera na miongozo ya matibabu ya malaria na vilevile kuhakikisha takwimu za TES zinatumika kufanya maamnuzi yenye tija katika kupunguza malaria nchini.

**BAJETI**
Dola za Marekani milioni 19.5

**MUDA**
Agosti 2018 – Agosti 2023

**MAENEO YA MRADI**
Mradi wa OMDM unatekelezwa nchi nzima yaani Tanzania Bara na Zanzibar

**MTEKELEZAJI**
RTI International

**MAWASILIANO YA USAID**
Chonge Kitojo
Mtaalam wa Usimamizi wa Mradi, Malaria
+255 746 700 832
ckitojo@usaid.gov

**MAWASILIANO YA MSHIRIKA**
Ssanyu Nyinondi
Mkuu wa Mradi, OMDM
RTI International +255
784 957 957
snyinondi@utm.rti.org

**KWA TAARIFA ZAIDI**
Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania

## Eneo la nne: Kuboresha utumiaji wa taarifa katika kufanya Maamuzi

Ili kuendelea zaidi katika njia za kutokomeza malaria, OMDM inatoa msaada wa kitaalaam kwa NMCP na ZAMEP kuimarisha uwezo wa watendaji kuchambua na kutafsiri takwimu kwa ajili ya matumizi katika kufanya maamuzi kulingana na taarifa zilizopo. Mbinu za kujenga uwezo za OMDM ni pamoja na (1) kuongeza idadi ya wataalam wa udhibiti na ufuatilaiaji wa mbu (entomologists), wataalam wa ufuatiliaji wa magonjwa, wataalamu wa TEHAMA, wachambuzi wa

takwimu na wataalamu wa sera kupitia kozi za muda mfupi na mrefu,  na ushauri endelevu wa kiutaalamu, ; (2) ushirikishwaji wa NMCP, ZAMEP na wafanyakazi wadau katika  kutekeleza na kufanyia kazi  maswala mbalimbali ya kiutafiti ya OMDM ; na (3) kutoa fursa na usaidizi kwa wafanyakazi wa NMCP na ZAMEP kuhudhuria mikutano na makongamano ya kitaifa, kikanda na kimataifa, kushiriki katika ziara za mafunzo na kuchapisha matokeo ya programu na mafanikio katika fasihi zilizokaguliwa na kuchapishwa na wataalamu wa malaria.